

Pambazuko

Toleo Namba 066

Jumatatu Machi 18-24 2024



**Majambazi waacha
bunduki, waingia
mitandaoni kupora**

●Wafanyakazi benki wakwapua bilioni 2.5/-



JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye
namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Wakati wa Rais Samia kuwa mkali zaidi

JUMATANO ya Machi 29, mwaka jana, Rais Samia Suluhu Hassan alionyesha hasira zake kwa umma kwa kutamka maneno makali.

Akipokea ripoti ya Mkaguzi na Mdhhibiti Mkuu wa Fedha za Serikali (CAG), jijini Dar es Salaam, Rais Samia alikerwa mno na kuwepo kwa kila dalili za rushwa, wizi na ubadhirifu ambazo zimesheheni ndani ya taarifa hiyo aliyokabidhiwa.

Katika uongozi wake wa miaka mwili, kwa mara ya kwanza, Watanzania na dunia walishuhudia namna ambavyo Rais Samia hapendi rushwa, wizi na ubadhirifu. Alifoka huku sura yake ikionekana “kuvaa” hasira.

Rais Samia alifika wakati akatumia maneno makali ya Kiingereza; “stupid” – akimaanisha upumbavu mkubwa kwa baadhi ya watendaji wa serikali ambao wamekuwa wakishindwa kutumia uzalendo katika kuwajibika, badala yake wamekuwa wakiamini dhamana zao ni chumo lao kwa manufaa binafsi.

Pamoja na Pambazuko kupongeza hasira hizo za Rais Samia, bado tunaamini kwamba hasira pekee hazitoshi kuwakemea Watanzania wengi kuacha rushwa, kujihusisha na ubadhirifu na hata matumizi mabaya ya dhamana walizokabidhiwa kwa niaba ya wananchi.

Rais Samia amekuwa sehemu ya utendaji wa serikali kwa muda mrefu, hivyo tunaamini anatambua wapi kuna mianya mingi ya rushwa ubadhirifu na uchafu mwingine ambao unachafua taswira ya serikali yake kwa umma wa Waanzania na dunia.

Kimsingi, wanaotenda maovu hayo, wanamchongea Rais Samia kwa wananchi, na kumuonyesha kwamba ni kiongozi asiyechukua hatua kunapotokea uchafu katika utendaji wa serikali.

Kama ambavyo wananchi wengi wanapendekeza Rais Samia kuchukua hatua kali; ikiwamo kuwatimua kazini na kuwafungulia mashtaka wote wanaiba mali za wananchi, nasi katika Pambazuko tunasisitiza kiongozi huyo wa nchi yetu kuchukua hatua kwa wote wanaomhujumu.

Kuiba mali ya umma ni dhambi kubwa mno, kwani inahusisha kudhulumu haki za idadi kubwa ya wananchi. Kuiba fedha za maendeleo maana yake ni kwamba mwizi huyo anakwamisha ujenzi wa barabara, anachelewesha kama siyo kuzuia kabisa ununuzi wa dawa katika hospitali na anakwamisha kuimarika kwa elimu ya watoto wetu.

Mwizi wa mali ya umma ni mbaya mno. Ni sawa kabisa na kuua watu kwa manufaa ya mtu binafsi na gharama za wengi.

Ndiyo maana katika nchi zingine, mwizi wa mali ya umma hupewa adhabu kubwa ikiwamo kunyongwa ili kuwa fundisho kwa watendaji wengine wenye tamaa ya kupata utajiri wa harakaharaka kwa mgongo wa fedha za maendeleo ya umma.

Pambazuko linamuomba Rais Samia sasa kuwa mkali zaidi kwa wezi wote wa mali ya umma na wale wanaotumia vibaya dhamana zao.

Sisi Pambazuko tuko tayari kumsaidia kwa njia tunazoweza ili kuifanya Tanzania ikome kuwa shamba la bibi.

ACT WAZALENDU



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ACT – Wazalendo, Tanzania Bara, Isihaka Mchinjita amepokelewa jana na viongozi na wanachama wa chama hicho huko mjini Lindi, mara baada ya kuwasili mjini humo. Hii ni mara ya kwanza kwake kurejea “nyumbani kwake” baada ya kuchaguliwa kwa nafasi hiyo, Machi 5, mwaka huu. (Picha na X.com).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko.tza@gmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



Ukitaka kufanikiwa zaidi, tembea, kutana na watu na kikubwa zaidi, zungumza nao. Kamwe usijifungie chumbani na kusubiri neema na heri kutoka popote. Kinyume na haya, utageuka kuwa mtu wa kulalamika na kuona waliofanikiwa kujawa “ushetani.” – Msemo wa Kichina.

Tangazo

Tuchangie

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako na wale wengine tuliwaomba kuchagua, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**

**Mhariri Mkuu,
Oktoba, 2023**

Changia Pambazuko liendelee

WAJUMBE wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko wameendelea kufuraha kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakitumia fedha, muda, ujuzi na rasilimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wazungumzaji wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote; wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokua zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili - miezi 15, mengi mazuri yamepatilana, mbali na kukuza Kiwahili, kuhabarisha, kupata maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeweza kusukuma watoto uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yamewekwa wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kuepusha majanga, kuponya majeraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kuimarisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa - na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili linazoe kuuza, lakini haukubaliani na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hiari ili kutoa mwanya kwa gazeti hili kuendelea kuufikia umma bure.

Sasa basi, endapo utapata kuchangia maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hatuna kikubwa wala kidogo; yote ni michango na ina thamani sawa ya "asante" kutoka kwetu.

Tuma mchango wako kutoka mtandao wowote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utatufikia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263

Ukituma mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandika: **Pambazuko Gazeti**. Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako - na wale wengine uliwaomba kuchagua, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263**.

Lipa kwa Simu

Lipa kwa kuscanner



Lipa kwa Namba

6 2 1 4 5 0 0

PAMBAZUKO GAZETI







Kikwete aibuka kidedea tuzo ya amani

Na Mwandishi WETU

ASILIMIA 60 za kura zilizopigwa mitandaoni, zimetosha kumtangaza Rais (mstaafu) wa Tanzania, Jakaya Kikwete kuwa mshindi wa tuzo ya amani Afrika.

Tuzo hizo ambazo hufanyika kila mwaka, zinazoandaliwa na Jarida la Uongozi Afrika (ALM), zikiwa na lengo la kutambua mchango wa Waafrika katika uongozi uliotukuka.

Katika mchujo wa mwaka huu, mbali ya viongozi wa nchi, pia wananchi wa kawaida wanaojitolea kutatua changamoto za jamii, walijumuishwa kwa kutajwa na wasomaji wa ALM.

Katika tuzo za mwaka huu, ambazo humtambua mshindi kwa mwaka uliopita, 2023 zilifanyika juzi – Machi 16, Mji Mkuu wa Ethiopia, Addis Ababa, ambako ndiko yaliko makao makuu ya Umoja wa Afrika (AU).

Tuzo za mwaka huu zinamtaja Kikwete kuwa kiongozi bora wa mwaka katika maeneo amani na usalama Afrika.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo Kikwete alishukuru kwa kutunukiwa tuzo hiyo na kuwasihia Waafrika wote kwenye nafasi za uongozi kutoa kipaumbele kwenye masuala muhimu ili kutatua changamoto zilizopo ikiwemo umasikini, changamoto ya chakula, mabadiliko ya tabianchi, magonjwa, ujinga, migogoro ya kisiasa na vita.

“Ukweli ni kwamba, ni kwa heshima kubwa ninakubali kupokea tuzo hii, naipokea siyo tu kwa ajili yangu, bali kwa niaba ya Waafrika wengine wengi, wawe ni viongozi wa kisiasa, wenye ushawishi kiuchumi, viongozi wa dini, wanachama wa vikosi vya usalama, watumishi wa umma, na wananchi wa kawaida ambao huamka kila siku na kuweka mchango wao kulifanya Bara la Afrika kuwa sehemu nzuri zaidi ya kuishi,” aliongeza



Kikwete akipokea tuzo yake

Kikwete.

Kikwete ametunukiwa tuzo hiyo kufuatia mchakato uliojumuisha mapendekezo ya majina pamoja na kura zilizopigwa mtandaoni kwa wale waliopendekezwa, huku akiibuka na ushindi wa asilimia 60.

Katika hatua nyingine Kikwete pia amepongeza juhudi zinazofanywa na Afrika katika kupiga hatua kimaendeleo, hususan mapinduzi makubwa katika kuboresha elimu na kuweka mkazo katika suala zima la kupatikana kwa chakula.

Watanania walioshinda tuzo hizo ni wawili ambao ni Kikwete pamoja na Jesca Nkwabi, ambaye ametunukiwa tuzo ya kiongozi bora wa mwaka kwenye kundi la vijana wanaofanya vizuri Afrika.

Tuzo hizi, ambazo zimeanza kupata umaarufu, hupambanisha majina ya viongozi wanaopendekezwa na wasomaji wa jarida hilo pamoja na watu wengine wanaopitia kurasa zake mitandaoni.

Vigezo vinavyotazamwa ni weledi wa kutumikia wananchi, kujali na kutatua changamoto zao, hasa wakati wa majanga na milipuko ya magonjwa.

Pia tuzo hizo hutazama mchango wa wanaopendekezwa katika kutatua mikwaruzano ya nchi na nchi na hata jamii.

Habari katika picha

Tunafuturu ...



*Ijumaa iliyopita –
Machi 15, Rais Samia
Suluhu Hassan alialika
wageni mbalimbali
kwenye futari
iliyoandaliwa katika
Viwanja vya Ikulu,
Tunguu, Zanzibar.
(Picha zote na Ikulu).*



Tanzania yang'ara utumishi wa umma

Na Mwandishi WETU

TANZANIA inatajwa kuwa miongoni mwa nchi chache za Afrika zinazoongoza kwa kutumia mifumo imara, na kisasa, inayosomana kirahisi kurahisisha mawasiliano kwa watumishi wa umma.

Hayo yamebainishwa jana jijini Dodoma na Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (ORMUB), Ridhiwani Kikwete, ambaye amesema sifa hizo zinafanya nchi zingine kujifunza Tanzania.

Kikwete amesema Tanzania imekuwa ikitumia mifumo hiyo ya kisasa imekuwa ikitumia kwa ufanisi na imekuwa “mwokozi” wa kutatua changamoto za kiutumishi kwa muda mfupi na kwa ubora wa kimataifa.

Mifumo inayorumika zaidi Tanzania katika kuendesha masuala ya kiutendaji kwa watumishi wa serikali – ikiwa ni pamoja na kupima ufanisi ni HCMIS, PEPMIS HR Assessment na mifumo mingine.

Ni kutokana na ufanisi mkubwa wa kufanikisha ubora wa mawasiliano na kupima utendaji wa watumishi wa umma, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Dkt. Joseph Mhagama amepongeza ORMUB kwa kubuni mifumo mbalimbali ya Tehama kwa lengo la kuboresha utendaji kazi serikalini.

Dkt. Mhagama amesema hayo jana wakati kamati yake ilipotembelea Ofisi ya Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, Sekretarieti ya Ajira na Tume ya Utumishi wa Umma kwa lengo la kupokea taarifa ya miradi mbalimbali inayotekelezwa na taasisi hizo.



Ridhiwan Kikwete akisisitiza jambo kwa wabunge

Aidha, Dkt. Mhagama amepongeza ORMUB kupitia taasisi zake kwa kufanya kazi kubwa ya kubuni na kusanifu mifumo ambayo ni muhimu na yenye lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kazi serikalini.

“Tulizoea kuona nchi za wenzetu zikibuni na kusanifu mifumo mahususi ya Tehama kwa maendeleo ya mataifa yao na wakati mwingine kutuuzia na sisi, lakini tumesikia na kuona hwa macho yetu uwezo mkubwa wa vijana wetu wa ndani ya serikali ambao wameunda mifumo muhimu kwa ajili ya serikali yetu, hakika haya ni mapinduzi makubwa yatakayoleta ufanisi unaozingatia haki na wajibu serikalini” alisema Dkt. Mhagama.

Kadhalika, Dkt. Mhagama ameisitiza ORMUB kuhakikisha mifumo yote ya Tehama iliyopo na inayoendelea kubuniwa na kusanifiwa, inakuwa endelevu ili kuboresha utoaji wa huduma kwa umma kwa njia ya kisasa na uhakika zaidi.

Afrika Kusini, Rwanda ni nchi zinazoelewa kutumia mifumo ya kisasa inayoongozwa na teknolojia zaidi katika kutoa huduma kwa wananchi wake, huku watumishi wa umma wakipimwa ufanisi wao kwa kutumia njia za kisasa zinazotawaliwa na mifumo ya kidijitali.

Kumbukizi

Magufuli akaidi Corona, alaumu ‘mabeberu’

Na Mwandishi MAALUM

JANA – Machi 17, ilikuwa kumbukizi ya miaka mitatu tangu kufariki – akiwa madarakani, kwa Rais wa Awamu ya Tano wa Tanzania, John Pombe Magufuli.

Katika kumbukizi hiyo, mengi yameandikwa, kuzungumzwa na kujadiliwa kwa namna tofauti; huku wakiwamo wanaosifu uongozi wake na wengine wakimweleza kinyume chake.

Wanaosifu wana sababu na wanatetea mtazamo wao, kama ilivyokuwa kwa wale wanaoeleza kuwa hakuwa kiongozi mzuri. Nao, kama ilivyokuwa kwa wanaosifu, wanasababu zao. Yote ni uhuru na haki ya kujieleza.


Katika mijadala hiyo, wanaosifu wanajikita kwenye sifa yake kuu ya kuwa mkali na msimamizi wa kile anachokiamini, hata kama kitakuwa na matokeo mabaya.

Hawa wanamsifu Rais Magufuli kwa ujenzi wa miundombinu; hasa barabara na madaraja, uthubutu wake wa kuhamia shughuli zote za serikali Dodoma, kuanza kwa ujenzi wa Bwawa la Julius Nyerere - lenye kuzalisha umeme, kufufua Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) na kuanza ujenzi wa reli yenye kasi, inayopitisha treni ya umeme (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza.

Miongoni mwa wanaopinga sifa za utendaji wa Rais Magufuli, wanaeleza mengi, lakini kubwa wanaloshikilia ni msimamo wake kwenye kukabili mlipuko wa ugonjwa wa Corona (Covid-19).

Hawa wanaeleza namna Rais Magufuli, msomi wa kemia ambaye aliamua kuacha “uhakika wa sayansi” na kuwa mpiga ramli, ambaye aliuaminisha umma kwamba ugonjwa huo ungeweza kuondoka kwa maombi, “kujifukiza” na zaidi sana, kuacha kuuogopa.

Katika kutetea hoja zake, Rais Magufuli alitamka bayana kauli kuu tatu ambazo zimewekwa kwenye historia



Hayati John Pombe Magufuli

kuhusu msimamo wake kwa mlipuko wa ugonjwa huo.

Tusitishane: “Corona siyo ishuru kubwa kwa sababu hata “ukimwi na malaria huua watu kama ilivyo kwa ajali. Kwa hiyo Watanzania wasiogope na wauchukulie ugonjwa huo kuwa ni wa kawaida tu.”

Corona ni kazi ya shetani: “Njia ya kupambana na kazi ya shetani ni kumtegemea Mungu. Kwa siye waumini, Mungu ni wa kumtegemea kwenye kila jambo, hivyo, kuushinda ugonjwa huo, ni kumkimbilia Mungu.”

Hapa Rais Magufuli, alimaanisha kuwa ugonjwa huo siyo suala la kisayansi, bali la kiroho. Kwa mtazamo wake, vita dhidi ya Corona ipiganwe makanisani na misikiti badala ya kwenye maabara na matibabu ya kisayansi - hospitalini.

Corona ni mkakati wa mabeberu: “Huu ugonjwa ni mapandikizi tu ya mabeberu, wanatuonea wivu, na sasa wanakuja na magonjwa ya ajabu ajabu.”

Kauli hizi za msimamo wa Rais Magufuli kuhusu janga la Corona, zilimfanya aonekane “kituko” mbele ya dunia, huku yeye akisisitiza kwamba ugonjwa huo, ni sawa na mafua, unaoweza kudhibitiwa kwa mchanganyiko wa viungo maarufu vya pilau.



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Wapigania ubunge wamharibia Rais Samia

Na Rashid Mtagaluka

KESHO Jumanne tunaadhimisha miaka mitatu tangu Samia Suluhu Hassan ale kiapo cha kuiongoza Tanzania – akiwa rais wake, kufuatia kifo cha ghafla cha mtangulizi wake, Dkt. John Magufuli.

Wakati huu tunapojiandaa kusherehekea maadhimisho hayo, wengine lazima tutafakari baadhi ya mabadiliko yaliyojitokeza kwenye kipindi hiki kifupi cha uongozi wake.

Ili kumtendea haki Rais Samia katika tathmini fupi ya uongozi wake, hatuna budi kurudi nyuma kidogo kutazama waliomtangulia walifanyaje na waliichajaje nchi.

Kwa kuchelea kutumia muda mrefu hoja yangu haitanzia kwa Rais Ali Hassan Mwinyi - mwaka 1985 alipokuja na Azimia la Zanzibar lililolegeza masharti magumu yaliyo kwenye Azimio la Arusha, hivyo kuruhusu kuwepo kwa soko huria kulikosababisha kufungua milango ya kiuchumi.

Na wala hoja yangu haitamulika zama za ubinafsishaji wa mashirika ya umma kwa namna ambayo wengi walishangazwa na uamuzi huo, lakini kwa kuwa ilikuwa ni uamuzi wa kiongozi mkuu wa nchi wa wakati huo, hakukuwa na mkosoaji aliyesikilizwa!

Pia hoja yangu siyo kukumbusha enzi ambayo Maabara Kuu ya Taifa ilipelekewa sampuli za vipimo na hatimaye tukatangaziwa mapapali, mafenesi, matikitimaji vilivyopewa majina bandia ya watu, kugundulika kuwa na vimelea vya Covid-19.

Ninachotaka kusema katika kipindi hiki kifupi cha uongozi wa Rais Samia, pamoja na kufanikiwa kuleta mabadiliko mengi chanya yakiwemo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii, lakini hoja yangu ni kundi dogo la wasaidizi wake, kujikita kutengeneza mitandao ya kusaka kura huko majimboni.



Rais Samia Suluhu Hassan

Kwamba serikali anayoongoza Rais Samia kwa kipindi cha miaka mitatu, imefanikiwa kurejesha utengamano wa kisiasa kupitia falsafa yake ya kuwezesha wanasiasa kuvumiliana kwa kuruhusu mikutano ya hadhara kufanyika.

Lakini zaidi na ambalo Samia linaweza kumfanya apate tuzo ya Mo Ibrahim yenye heshima kubwa Afrika na duniani baada ya kumaliza muda wa uongozi, ni hili la hivi karibuni kuruhusu chama kikuu cha upinzani nchini kuandamana nchi nzima!

Hata hivyo, Rais Samia ana kibarua cha kuendelea kutafakari kama wateule wengi aliowaamini kufanya kazi ya kuwatumikia wananchi wamekidhi matarajio yake na matarajio ya Watanzania, au wengi wao wanawaza ubunge 2025 na urais 2030?

Kupata majawabu ya hili, rais hana haja ya kupiga ramli, kutumia wala darubini kali, ziara pekee za Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Paul Makonda zinaweza kumpa majibu.

Hakika Makonda amewaumbua watendaji wengi na hata wateule wa moja kwa moja wa rais, ambao imebainika wamebweteka, huku wakiwaza kuingia mjongoni mwaka kesho. Hawafanyi kazi.

Rashid Mtagaluka ni Mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari: 0784 438 546 au email: mtagaluka@gmail.com

Habari

Majambazi waacha bunduki, waingia mitandaoni kupora

Na Mwandishi WETU

NYAKATI za kutumia silaha za moto kupora pesa kutoka kwenye taasisi za fedha na kwa watu binafsi, zinaonekana kupitwa na wakati, na sasa mitandao ya kijamii inatumika kutekeleza uporaji mkubwa.

Hayo yamebainika kupitia ripoti iliyochapishwa hivi karibuni na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ambayo inaonesha kuwa hakukuwa na tukio lolote la uporaji fedha kwa kutumia silaha lililoriipotiwa mwaka jana, 2023.

Lakini kwa upande mwingine, takribani shilingi bilioni 10.3 ziliibwa kutoka taasisi za fedha na kwa watu binafsi kupitia wizi wa mtandaoni huku karibu nusu ya kiwango hicho kikubwa kikipitia miamala ya simu za mkononi.

Ripoti hiyo imeorodhesha wizi unaofanywa na wafanyakazi ndani ya benki; kughushi hundi, wizi kwenye mitandao ya simu na kwenye intaneti na wizi kupitia mashine za kutolea fedha (ATM), kuwa ndio matukio yanayoongoza katika wizi wa fedha kupitia mitandao.

Pia, katika kipindi hicho hakukuwa na tukio lolote la uporaji fedha la ujambazi, jambo ambalo lilikuwa ni kawaida miaka michache iliyopita.

Kwa mujibu wa BoT, wakati wizi kupitia miamala ya simu za mkononi ikiongoza katika matukio ya wizi mitandaoni - kwa kuhusisha shilingi bilioni 4.9, wizi unaofanywa na wafanyakazi ndani ya benki, unafuatia ukihusisha takribani shilingi bilioni 2.5.

Wizi kupitia hundi za kughushi ulihusisha kiasi cha shilingi bilioni 1.02, huku aina nyingine za wizi mitandaoni zikihusisha kiasi cha shilingi bilioni 1.15.

Hali hii ni tofauti kabisa na mambo yalivyokuwa miaka michache iliyopita, mathalani, kwa mujibu wa takwimu



Waziri wa Fedha - Dkt. Mwigulu Nchemba

kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), hakukuwa na tukio lolote la wizi kwenye mabanki lililoriipotiwa mwaka huo, huku kukiwa na matukio 78 tu yakihusisha uhalifu wa noti bandia.

“Idadi ya makosa ya uhalifu wa kifedha nchini ni 905. Mikoa ya Kipolisi yenye idadi kubwa ya makosa ni Ilala (163), Kinondoni (108), Temeke (52), Dodoma (47) na Kilimanjaro (45).

Makosa yaliyoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ni kugushi (744), noti bandia (78) na wizi katika mashirika ya umma (50),” inasema NBS katika ripoti hiyo.

Hali hii inaonesha kuwa hata wezi nao sasa wamegeuka kutoka kwenye matumizi ya nguvu na silaha za moto ili kujipatia fedha na kuanza kuitumia teknolojia kufanya uhalifu.

Akionya kuhusu hilo, Tusekelege Joune, Mkurugenzi wa Umoja wa Mabenki Tanzania, amewataka wananchi kuwa waangalifu hasa wanapotakiwa kutoa taarifa kuhusu mifumo ya uhifadhi fedha katika akaunti zao kwenye simu au benki.

Akizungumza na UTV hivi karibuni, Joune alisema kuwa wapo watu ambao wanakuwa wepesi kutoa taarifa zao za

Majambazi waacha bunduki

Inatoka Uk. 10

mifumo ya kifedha kwenye simu au akaunti za benki wanapopigiwa simu.

“Utakuta mtu anapokea meseji au anapigiwa simu na mtu anayejitambulisha kama mfunyakazi wa mtandao wa simu anayoitumia au benki na kutakiwa kutoa neno lake la siri. Nawasihii wananchi wasifanye hivyo kwa sababu hakuna benki au mtandao wa simu utakupigia na kukuomba taarifa hiyo,” alisema.

Ili kukabiliana na hali hiyo, Jouné alisema jambo la kwanza linalopaswa kufanywa na watoa huduma za kifedha ni kuimarisha mifumo yao ya kimtandao kwa kuiweka ulinzi madhubuti.

“Na hilo ndilo linalofanyika hivi sasa kwani benki nyingi na kampuni za simu zinawekeza kiasi kikubwa cha fedha kwenye kuimarisha mifumo yao ili isiwe rahisi kwa wahalifu kuingilia,” anabainisha.

Kwa mujibu wa wataalamu kutoka katika mabenki na mitandao ya simu za mikononi, matatizo mengi hutokea wakati mteja anapotoa neno au namba yake ya siri kwa mtu mwingine asiyehusika.

Hivyo, wateja wa kampuni za simu na benki wameshauriwa kutotoa namba zao za siri kwa mtu asiyehusika na wahakikishe wanabadili maneno hayo ya siri mara kwa mara ili kuzuia uwezekano wa mtu kuikariri na kuingia kwenye akaunti yako bila ridhaa yako.

Joshua Mwangasa, Mkuu wa Kitengo cha Uchunguzi wa Makosa ya Kimtandao kutoka Jeshi la Polisi Tanzania, amesema kuwa ripoti hiyo ya BoT inaonesha jinsi teknolojia inavyoweza kubadilika haraka.

Anabainisha kuwa miaka michache iliyopita, Jeshi la Polisi lilikuwa likikabiliana na aina za uhalifu ambazo zilikuwa hazibadilikibadiliki, lakini hali hiyo ni tofauti sana hivi sasa kwani teknolojia imesababisha mabadiliko ya

BENKI KUU YA TANZANIA
2 MIRAMBIO STREET
11884 DAR ES SALAAM TANZANIA
Simu ya Mdomo: +255-22-2234494/5/7
+255-22-2235531
Anwani ya Simu: "BENKUU"



BANK OF TANZANIA
2 MIRAMBIO STREET
11884 DAR ES SALAAM
TANZANIA
Phone: +255-22-2234494/5/7
Direct Line: +255-22-2235531
Fax No: +255-22-2234189
CABLE: "BENKUU"

Bankchamba
Ref. No.

FA-53/359/01/25

5th March 2024

**TO: ALL BANKS AND FINANCIAL INSTITUTIONS
ALL PAYMENT SYSTEMS PROVIDERS**

RE: SUBMISSION OF INFORMATION ON FRAUD INCIDENCES

Reference is made to the Bank of Tanzania Circular Letter No. FA-235/519/01 dated 27th December 2012, regarding the captioned subject.

The Bank of Tanzania wishes to share with you a consolidated summary of losses occasioned by fraud incidences in the banking sector for four quarters as indicated in the table. We expect that the feedback will be used to improve internal controls with the view to minimize future losses due to frauds.

NATURE OF FRAUD	March 2023 TSh	June 2023 TSh	September 2023 TSh	December 2023 TSh	% change from April 2023 to Dec 2023
Internal staff fraud	431,921,442	227,317,380	1,330,299,922	448,394,225	-63
Mobile and internet banking (including cyber-attacks)	1,449,067,075	674,062,254	901,667,410	1,634,767,274	84
ATM Card Skimming	57,464,796	424,144,753	79,444,255	139,871,259	-60
Forged Cheques and TDS	34,000,000	954,914,901	20,900,000	11,300,000	-46
Armed Robbery	0	0	0	0	0
Others	324,664,160	214,894,797	202,937,241	345,113,403	14
TOTAL	2,497,164,467	2,855,026,384	2,474,470,888	2,441,148,362	-1

Please be informed accordingly.

Yours faithfully,
BANK OF TANZANIA


Njiru
Head of the Unit


Dabaka, A. A. M.
Head of the Unit

DIRECTORATE OF FINANCIAL SECTOR SUPERVISION

kasi hata kwenye uhalifu.

“Uhalifu unakuja na taswira mpya, jinsi ambavyo teknolojia inabadilika, basi, uhalifu nao unakuwa na mabadiliko makubwa. Niwashukuru BoT kwa ripoti hii kwa sababu kwa taswira iliyooneshwa inatupa namna ambavyo sisi tunalazimika kubadilika pia,” anasema.

Anasema kitengo cha kukabiliana na uhalifu mtandaoni kutoka Jeshi la Polisi, kina mikakati mingi iliyopanga kuifanya ili kukabiliana na aina hiyo ya uhalifu huku akitaja moja ya mikakati hiyo kuwa ni kutoa elimu kwa umma kuhusiana na uhalifu huo na jinsi ya kujikinga nao.

Anasema kwa kiasi kikubwa uhalifu auhusishi uvamizi mkubwa wa mifumo ya kitaifa, bali ni utapeli unaotokana na wateja huku kutokuwa na taarifa sahihi kuhusiana na akaunti zao.

Mwangasa aliyataka mabenki kuweka
Inaendelea Uk. 12

Habari

Majambazi waacha bunduki

Inatoka Uk. 11

mifumo imara ya ulinzi kwenye mitandao yao ili kuhakikisha kuwa wahalifu hawawezi kuiingilia kwa urahisi.

Anabainisha kuwa mwaka jana Jeshi la Polisi lilipokea matukio 1,369 ya uhalifu mitandaoni na nusu ya matukio hayo yameshashughulikiwa, huku baadhi yake yakiwa bado yako mahakamani.

“Makosa 139 tayari yalishapata ushindi mahakamani. Yapo matukio mengi ambayo kesi zake bado zinaendelea,” anasema akibainisha kuwa makosa mengi yanahusisha matukio ya utapeli kama vile mtu kupigiwa simu au kupelekewa ujumbe akitakiwa kutuma fedha kwenye namba fulani.

Kachero huyo anaongeza kuwa ili kuhakikisha ulinzi wa kimtandao unawafikia Watanzania wengi, Jeshi la Polisi lina mkakati wa kuwafundisha watendaji wengi zaidi na kuwapatia utaalamu wa kukabiliana na aina hii ya uhalifu.

“Tumeanza kuandaa mfumo maalum wa kuwafundisha watu ili utaalamu huu ufike hadi ngazi ya kanda zote za kipolisi nchini na wengi zaidi wapate ujuzi wa namna ya kukabiliana na kukomesha kabisa uporaji unaotumia mitandao,” anasisitiza.

Tanzania salama mitandaoni

Hata hivyo, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Tehama Tanzania, Dkt. Nkundwe Mwasaga, amesema hali ya usalama mtandaoni Tanzania ni nzuri sana na ndio maana wafanyabishara wengi kutoka nje wanavutiwa kuja kuwekeza nchini.

Aliyasema hayo hivi karibuni jijini Dar es Salaam wakati akitangaza kufanyika kwa kongamano la usalama wa kimtandao litakalofanyika mwanzoni mwa mwezi ujao jijini Arusha.

Dkt. Mwasaga alibainisha kuwa tafiti zinaonesha kuwa Tanzania ni ya pili kwa usalama wa mtandaoni miongoni mwa nchi za Afrika na ndio maana kampuni



Sampuli ya fedha za Tanzania

kubwa za tehamu zinavutiwa kuja kuwekeza nchini.

Kwa mujibu wa Dkt Mwasaga, kati ya mambo yatakayojadiliwa katika kongamano hilo ni umadhubiti wa kimtandao katika uchumi wa kidijiti.

“Tutajadiliana na wataalamu kutoka ndani ya nchi na kutoka nje ya nchi masuala yote yanayohusiana na usalama wa kimtandao kwa sababu sote tunafahamu kuwa suala la usalama lisipokuwa vizuri, mengine yote tunayoyafanya kwenye mapinduzi ya kidijitali hayatafanikiwa na hasara zitakuwa kubwa zaidi,” alisema Dk. Mwasaga.

Mwanaidi Mwasemi, mtaalamu wa mifumo ya usalama ya kuendesha mitandao ya kijamii kutoka Kampuni ya ITwind ya Dar es Salaam, amesema kuwa wakati umefika sasa kampuni za simu kuwa na mifumo ya ulinzi inayoendana na wakati na kukubali kuwekeza zaidi ili kukabili wizi ambao unaelekea kushamiri.

“Pamoja na sifa kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye usalama mkubwa wa kimfumo ndani ya mabadiliko makubwa ya teknolojia na kimtandao, serikali na vyombo vya usalama havipaswi kubetekwa, kwani mabadiliko ya uhalifu wa mitandaoni yanafanyika kila dakika,” anaongeza mtaalam huyo.

Duni ashinda majaribu, astaaifu kwa kishindo

Na Mwandishi WETU

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo, Juma Duni Haji maarufu “Babu Duni,” amestaafu uongozi.

Kustaafu kwa mwanasiasa huyo nguli wa siasa za mageuzi ndani ya chama chake, kulihitimishwa katika Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam mbele ya wajumbe wa mkutano mkuu wa chama hicho kinachoendelea kujiimarisha. Mkutano huo ulifanyika Machi 5 mwaka huu.

Hata hivyo, mkongwe huyo wa siasa za Zanzibar na Tanzania Bara, alitetea nafasi yake, ingawa siku moja kabla ya uchaguzi wa mwenyekiti wa chama hicho, alijiondoa kwenye kinyang’anyiro hicho na kumuunga mkono mshindani wake pekee, Othman Masoud Othman.

Ikumbukwe kuwa Duni alirithi kiti hicho baada ya Maalim Seif Sharif Hamad kufariki dunia mwaka 2021, na chama hicho kuitisha uchaguzi kuziba nafasi hiiyo.

Kabla ya kujitoka kwenye mchakato huo na kumwachia Othman, tayari kulikuwa na sintofahamu na hisia mbalimbali ndani na nje ya chama kuwa huenda ukatokea mpasuko mkubwa ambao ungegigawa chama hicho ukihusisha wale waliokuwa wakimuunga mkono Babu Duni kwa upande mmoja na mwingine Othman ambaye ni maarufu kwa jina la “Omo.”

Hatua ya Babu Duni kujitoka na kumwachia Othman agombee peke yake, kimezidi kumjengea umaarufu na heshima kubwa ndani ya chama hicho na kumfanya astaaifu kwa kishindo.

Katika hotuba yake kwa wajumbe wa mkutano huo mkuu Machi 5 mwaka huu, Babu Duni aliasa kwamba ili kukishinda Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika uchaguzi, ni lazima kuwe na umoja na mshikamano na kukataa kugawika kwa ujanja wowote ule.

Duni ambaye ni mwenyekiti wa tatu



Babu Duni

wa chama hicho tangu kilipoanzishwa mwaka 2014 ,akitanguliwa na Anna Mgwira, Maalim Seif Sharif Hamad (wote marehemu), aliyasema hayo wakati akihitimisha uongozi wake kwa kuwahutubia wajumbe, huku akiweka bayana kwamba yupo tayari – wakati wowote kutumika katika ngazi za ushauri ili chama “kisiende kombo.”

Akiwahutubia wajumbe hao, alisisitiza mshikamano, umoja na zaidi kufuata sheria, kanuni na taratibu walizojiweka ndani ya chama chao ili kuiondoa CCM kwenye usukani wa madaraka katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwaka keshi, 2025.

“Wajumbe waliomo katika ukumbi huu ni wanachama waliotoka katika makundi mbalimbali na maeneo mbalimbali na kabila mbalimbali. Kuna baadhi yetu tulitoka kwenye vyama vingine, kuna wengine kati yetu ni wapya kabisa wala hawakuwahi kuwa wanachama, wengi wao wakiwa vijana wa rika mbalimbali, wamejumuika nasi, chini ya dhamira moja tu ya kushikilia dola. Ifahamike kuwa sote tupo hapa tukiwa wahanga wa mfumo wa siasa za hovyoyo za CCM na utawala wake...”

“Kinachotukutanisha hapa na kujenga udugu kama vile ni watu wa ukoo mmoja ni dhamira yetu ya kuwatumikia wananchi na kuleta maendeleo wanayoyalilia miaka

Inaendelea Uk. 14

Habari**Duni ashinda majaribu, astaaifu kwa kishindo***Inatoka Uk. 13*

nenda rudi...

“Na hapa iwe kwamba linapompata mmoja wetu liwe la msiba au la furaha, sote hushikamana kulisimamia au kulishughulikia kiukoo....

“Mshikamano wetu huu huitwa kama gundi linalotutofautisha na wengine chini ya dhamira ya kudai mabadiliko ya kidemokrasia nchini na kutetea kupata haki zetu za kuzaliwa kama wengine...

“Umoja na mshikamano huo lazima tuudumishe ndipo tutafanikiwa kuishinda CCM. Tukatae kugawiwa kwa ujanja wowote ule,” alisema Duni.

Katika hilo, aliongeza kuwa ACT-Wazalendo ni sawa na ukoo uliotakiwa kuwaunganisha Watanzania ili wakatae uonevu, kudhalilishwa, kunyanaswa, kubaguliwa au maovu mengine yanayofanywa dhidi ya heshima ya utu wa binadamu.

Mkongwe huyo wa siasa za mageuzi, alisisitiza kuwa katika kuiongoza taasisi yoyote ile, lazima kuwepo mgawanyo wa kazi ambao huzaa mfumo wa utawala katika taasisi husika.

“Kwa kawaida matendo hayo huwa yamewekewa sheria, Kanuni, au utaratibu maalumu, utaratibu huo huwekwa katika kumbukumbu zinazomlazimu kila mwanataasisi kuzijua na kuzifuata. Kuacha kufuata matendo hayo hufuatana na hatua za kinidhamu ili kulinda mfumo mzima uendeleo kuwepo na hivyo kuepusha kutovurugika kwa taasisi,” aliongeza Babu Duni.

Duni aliwaeleza wajumbe hao kuwa kwa sasa jambo kubwa lililo mbele yao ni uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu, hivyo hawana budi kuwajua wapiga kura wao na baada ya hapo walinde kura zao na baadaye kulazimisha kupatiwa ushindi.

“Lazima tuwajue wapiga kura wetu na baada ya kupiga kura, tulinde kura zetu na kulazimisha kupatiwa ushindi. Mabadiliko ya sheria za uchaguzi uliofanyika unatupa matumaini ya kuwepo uchaguzi huru na

**Othman Masoud Othman**

wa haki. Tukajiandae kwa kuunda timu za ushindi kwa kila kijiji, mtaa na kitongoji,” alisisitiza.

Mwanasiasa huyo mkongwe ambaye wakati wa vuguvugu la ushirika wa vyama vya upinzani (Ukawa), alijiunga na Chadema akitokea CUF na baadaye kuwa mgombea mwenza wa chama hicho kikuu cha upinzani nchini mwaka 2015, alisema historia inaonesha wakishirikiana kwa ukweli na vyama vingine vya upinzani, watapata mafanikio makubwa dhidi ya CCM.

“Uchaguzi wa mwaka 2015 ni ushahidi tosha, kuna majimbo 28 tungeunganisha na kuwa na mgombea mmoja, basi vyama vyetu vingepata ushindi katika majimbo hayo na zaidi ya majimbo 43 kura zetu zimepishana kwa asilimia ndogo kabisa.

“Hivyo natoa wito na kuwajulisha viongozi wenzangu kuendeleza jitihada hizi kuwa na umoja wenye nguvu, usawa, haki na urari sawa kwa kila chama kwa masilahi ya Watanzania na taifa kwa ujumla,” alisema.

Babu Duni amekuwa mwanasiasa mwenye historia iliyotukuka, hasa kwa kuzingatia kwamba “amekuwa akipambana na hata kuhatarisha maisha yake, kwa kupigania haki na usawa.



Tangaza na **Pambazuko**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.

Kwa bei nafuu sana

0744 768 263 au

Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Habari katika picha

Hongera Wanawake



Wafanyakazi wanawake wa NSSF Mkoa wa Arusha, wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani – Machi 8. (Picha na NSSF).

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, akitangaza kuzinduliwa kwa programu maalum ya kuwawezesha wanawake kwa ujuzi (mentorship) iliyopewa jina la 'HE4SHE.'Hafta hiyo ilifanyika Arusha wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani – Machi 8. (Picha na CRDB).



Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi, akipokea tuzo ya utendaji uliotukuka kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan ikiwa ni kuhitimisha Siku ya Wanawake Duniani – Machi 8. Shughuli hiyo iliyofanyika Dar es Salaam, iliandaliwa na Mwananchi Communications kutambua mchango wa wanawake nchini. Kulia ni Waziri wa Habari, Nape Nnauye na kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mwananchi, Bakari Machumu. (Picha na Ikulu).

Dira ya Taifa 2050; tunapanga kushindwa?

Na Mwandishi WETU

MIPANGO ya kiuchumi ya nchi inaongozwa na Dira ya Taifa ili kufikia malengo yanayokusudiwa kwa kipindi fulani.

Hivi sasa Tanzania inakamilisha utekelezaji wa Dira ya Taifa ya mwaka 2025.

Utaratibu huu wa kuwa na Dira ya Taifa ulibuniwa mwishoni mwa uongozi wa awamu ya pili chini ya Rais Ali Hassan Mwinyi na kuanza utekelezaji katika awamu ya tatu, wakati huo rais akiwa Benjamin Mkapa.

Dira ni chombo cha kuongoza mwelekeo wa maendeleo kwenye nyanja zote katika taifa katika kipindi cha muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

Ndio maana utekelezaji wa Dira ya Taifa hugawanywa katika vipindi vya miaka 25, miaka mitano na hata mwaka mmoja mmoja.

Katika miaka 25, kunakuwa na lengo kuu la jumla linaloonesha maendeleo ya nchi yanapaswa kufikia wapi katika kipindi hicho.

Ili kulifikia lengo hilo utekelezaji wa mipango hiyo ya maendeleo hugawanywa katika kipindi cha miaka mitano mitano.

Ndani ya kila miaka mitano, kunakuwa na mpango wa mwaka mmoja mmoja ambao hutekelezwa kupitia bajeti katika mwaka wa fedha husika.

Hivyo, kimsingi, yale tunayoeleza katika bajeti ya kila mwaka, ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya miaka mitano na miaka 25.

Mchakato wa kuandaa dira ya maendeleo nchini ulianza mwaka 1994, mwaka mmoja kabla Rais Mkapa hajaingia madarakani.

Mchakato huo ulikamilika na dira kupitishwa mwaka 1999 na utekelezaji wake ukaanza kupitia bajeti ya waka wa fedha uliofuata, 2000.



Wasiri wa Mipango - Prof. Kitila Mkumbo

Kwa kawaida, uandaaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa unapaswa kuhusisha makundi yote katika jamii, kwani hakuna kundi ambalo halihusiki na maendeleo.

Pamoja na hayo, ushirikishwaji huu mpana unalenga kuipatia dira hiyo uhalali wa kuwa chombo kinachotumika kwa ajili ya maendeleo ya wote.

Kwa maana hiyo, utekelezaji wa dira hiyo uhusisha kila Mtanzania. Dira inapoweka malengo kuwa ifikapo mwaka fulani kila mwananchi awe na maisha bora.

Hakuna mtu mwingine kutoka mahali pengine ambaye atakuja kutekeleza mipango ya kumfanya kila Mtanzania awe na maisha bora, isipokuwa mwananchi mwenyewe.

Ukiacha ushirikishwaji wa wananchi wote, jambo jingine kubwa inapoandaliwa Dira ya Taifa, ni tathmini ya dira inayomaliza muda wake.

Ni lazima kufanya tathmini ya dira inayomalizika ili kupima mafanikio yake kwa lengo la kuhakikisha kuwa yanaandelezwa.

Pia, tathmini ya dira inayomaliza muda

Habari

Dira ya Taifa 2050; tunapanga kushindwa?

Inatoka Uk. 17

wake, ni muhimu ili kubaini mambo yaliyokwaza utekelezaji wa dira hiyo.

Mambo haya yanawezesha kuandaa dira mpya ambayo inatoa suluhisho kwa vikwazo na changamoto zozote zilizoibuka wakati wa utekelezaji wa dira inayomaliza muda wake.

Kwa kuwa mwaka 1994 ilipoandaliwa dira ya kwanza ya maendeleo hakukuwa na dira nyingine kabla yake, naamini tathmini ilifanyika kwa kuzingatia hali ya uchumi wakati huo na kuona ni wapi Tanzania inapaswa kuelekea.

Ni lazima tathmini ilifanyika kwa sababu bila hiyo ingekuwa vigumu kuweka vigezo vya nini kinatakiwa kufanyika na kifanyike vipi ili kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa.

Lakini, kitu cha ajabu ni kuwa mchakato wa kuandika Dira ya Taifa ya mwaka 2050 umeshaanza huku tathmini ya Dira ya Mwaka 2025 ikiwa haijakamilika.

Kazi ya kufanya tathmini hiyo ilitolewa kwa taasisi moja ya utafiti wa masuala ya

umasikini Tanzania, inayoitwa REPOA, lakini hadi wiki iliyopita ripoti mahsusi ya tathmini ya utekelezaji wa Dira ya Taifa 2025 ilikuwa bado haijakamilika.

Kuanza kuandaa mipango mipya bila kujua vigezo hivyo ni sawa na kufanya mapishi bila kuwa na viungo muhimu. Kuna hatari ukapika mchuzi ambao ladha yake haitajulikana vizuri.

Hii ina maana kuwa nchi inapoanza kupanga Dira ya 2050 bila ya kuwa na tathmini ya dira inayomalizika, ni sawasawa kabisa na kupanga kushindwa.


Dira inayomalizika ilikuwa na malengo matano makubwa.

Lengo la kwanza lilikuwa ni kuleta maisha bora kwa Watanzania wote. Chini ya dira ihiyo ilipangwa kuwa hadi kufikia mwaka 2025, kila mtanzania awe na maisha bora na pasiwepo ma Mtanania masikini.

Dira lilenga uwepo wa huduma bora za afya, elimu, maji, miundombinu, umeme, skimu za umwagiliaji na huduma nyinginezo za kiuchumi na kijamii.

Lakini, ni dhahiri kuwa hayo

Endelea Uk. 19





Dira ya Taifa 2050; tunapanga kushindwa?

Inatoka Uk. 18

hayajatimia kwa sababu huduma za jamii bado ni duni katika maeneo mengi na idadi ya masikini nchini, bado ni kubwa na kiwango cha umasikini ni kikubwa katika maeneo mengi.

Lengo la pili lilikuwa ni kuhakikisha kuwepo wa amani, utulivu na umoja. Utulivu wa kisiasa ni moja ya mambo ambayo yalilengwa kufikiwa ili kuwa na nchi yenye amani ya kweli.

Hivi sasa tunashuhudia mivurugano ya kisiasa inayoendelea nchini. Chadema na vuguvugu lao na madai ya katiba mpya na mabadiliko ya sheria za uchaguzi, huku ACT-Wazalendo ikieleza dhamira yake ya kujitoa katika serikali ya umoja wa kitaifa huko Zanzibar.

Tatu Dira ililenga kujenga utawala bora nchini. Sote ni mashahidi jinsi hata viongozi waliopo madarakani

wanavyoibua mambo ambayo yanaonesha kutokuwepo kwa utawala bora.

Lengo la nne lilikuwa ni kuhakikisha uwepo wa jamii iliyoelimika na yenye kujifunza. Sote tu mashahidi jinsi elimu yetu ilivyoendelea kuwa kitu cha majaribio miaka nenda miaka rudi.

Tano tulipanga kupitia Dira ya 2025 kuhakikisha Tanzania inakuwa na uchumi imara na shindani kwa mataifa mengine. Hili ni kama limeshindikana.

Nchi inajinasibu kuwa inajenga uchumi wa viwanda, lakini hadi leo bado tunatumia sehemu ndogo ya soko la Marekani kupitia AGOA kwa sababu hatuna viwanda vya kutosha kuzalisha bidhaa kwa ajili ya soko hilo.

Tukutane wiki ijayo ambapo baada ya kufanya tathmini binafsi na kuleta mapendekezo ya nini kinapaswa kupewa msisitizo kwenye Dira ya Taifa ya 2050.

Tunza mazingira yakutunze



Mwakilishi wa Kampuni ya Rentco yenye makao makuu yake, Nairobi Kenya, Doris Nyawira akishiriki kwenye shughuli ya kupanda miti katika Msitu wa Kisarawe, Pwani jana ikiwa ni ushuhuda wa urithi wa kudumu wa Wangari Maathai, raia wa Kenya na mwanamzingira anayeheshimika duniani. Raia wa Kenya wanaoishi na kufanya kazi Dar es Salaam, walikutana na kuazimia kumuenzi kwa kutetea uhifadhi wa mazingira bila kujali mipaka. (Picha na Ubalizi wa Kenya).

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa msunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

